1. LAZIMA: SEHEMU A; FAS

a. Soma kifungu kifuatacho kish

Lulu, mwanangu tulia,

Wiwi mtoto lala, mvua imekuja

Si uongo hata na miti huichangamkia

Mvua, hakuna haja ya kuelezwa,

Lulu mwana tulia,

Wiwi mtoto lala, mvua imekuja.

i. Tambua kipera hiki. (alama 1)

**Bembelezi/ bembea/pembejezi/bembe**

**ii.** Fafanua majukumu ya kipera hiki. (ala

Huongoa watoto walale.

Huonyesha hisia za walezi k

Huonyesha maisha ya walez

Huonyesha kiwango cha uch

Huwa njia ya kuwasilisha uju

Hueleza mtazamo wa jamii k

Ni njia ya kutoa malalamiko.

Hutumiwa kutumbuiza watoto.

Hutoa ahadi kwa watoto wakit

Huisifu jamii

21 copies Premeca 2024

## MWONGOZO PP3

### 1. LAZIMA: SEHEMU A; FASIHI SIMULIZI

**a. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Lulu, mwanangu tulia,

Wiwi mtoto lala, mvua imekuja

Si uongo hata na miti huichangamkia

Mvua, hakuna haja ya kuelezwa,

Lulu mwana tulia,

Wiwi mtoto lala, mvua imekuja.

i. Tambua kipera hiki. (alama 1)

**Bembelezi/ bembea/pembejezi/bembe**

**ii.** Fafanua majukumu ya kipera hiki. (alama 9)

Huongoa watoto walale.
Huonyesha hisia za walezi kuhusu uhusiano wao na wazazi.
Huonyesha maisha ya walezi.
Huonyesha kiwango cha uchumi cha wazazi
Huwa njia ya kuwasilisha ujumbe kutoka kwa mlezi.
Hueleza mtazamo wa jamii kuhusu watoto.
Ni njia ya kutoa malalamiko.
Hutumiwa kutumbuiza watoto.
Hutoa ahadi kwa watoto wakitenda mema.
Huisifu jamii inayojua malezi ya watoto.
Humpa mtoto matumaini ya hali nzuri ya maisha.
Hukashifu sifa mbaya ya watoto kv kulia.

Huliwaza watoto kwani huimbwa kwa sauti tamu na taratibu, nyepesi na nyenyekevu ili aache kuksirika. **Zozote 9**

b. Jadili matatizo ambayo mtafiti angekumbana nayo katika utafiti wa kipera hiki. (alama 10)

- Kushukiwa na jamii kwamba unawapeleleza
- Kunyimwa ruhusa na vyombo vya dola na kuingiliwa bila sababu katika kazi yake.
- Watendaji kutaka pesa kama malipo, vinywaji ama vitu vingine kama nguo. Ikiwa mtafiti hana pesa utafiti utakwama.
- Kutomaliza kazi kwa wakati unaotarajiwa na kutopata wakati wa kuhoji watu wengi na basi kutopata habari za kutosha.
- Matatizo ya usafiri na mawasiliano. Iwapo anahitaji kukusanya habari katika maeneo yasiyo na miundo msingi bora.
- Vikwazo vya kidini –baadhi wanafikiri Fasihi Simulizi imepitwa na wakati na inaweza kupalilia mambo yanayoenda kinyume na imani zao. Wanaweza kukataa kuimba baadhi ya nyimbo au kuhusu miviga
- Kupotea au kuharibiwa kwa vifaa vyao
- Mtazamo hasi wa wanajamii kuhusu ujazaji hojaji; inahitaji wanaojua kusoma& kuandika
- Uchache wa wataalamu na wazee wenye habari ya kutegemewa.
- ukosefu wa usalama. Huenda akavamiwa kwa sababu ni mgeni.
- matatizo ya kibinafsi km ugonjwa
- wadhamini huenda wakaamua wenyewe mahali na mada ya uchunguzi.
- Bei ya vifaa vya kuhifadhi dawa na usafiri ni ghali
- Vifaa vya kuhifadhia data vinaweza kupata virusi na basi kupoteza habari yote.
- Kutodhibiti hadhira na kuishia kuhojiwa badala ya yeye kuhoji.
- Tatizo la lugha. Ikiwa mtafiti hana ufahamu wala mkalimani wa lugha ya wahojiwa itakwamiza utafiti.
- Msamiati mwingine ni vigumu kutafsiri kutoka lugha chanzi hadi lugha pokezi.

**Zozote 10**

**SEHEMU B: TAMTHILIA. Bembea ya Maisha : Timothy Arege**

**Jibu swali la 2 au 3**

**2.** Jadili nafasi ya mwanamke katika Tamthilia ya Bembea ya Maisha. (alama 20)

Haya ni maudhui yanayonyesha namna mwanamke amesawiriwa katika tamthilia ya Bembea ya Maisha.

**Mwerevu** na mwenye maarifa. Kwa mfano, katika uk. 6 Kiwa anasema kuwa Sara amebarikiwa na watoto wenye akili nzuri. Wote wamehitimu vizuri na kuleta faraja. Tunaona Neema amesoma na kuhitimu Chuo kikuu na ana kazi nzuri. Asna na Salome vilevile wamefanikiwa kusoma hadi Chuo kikuu. Salome alipita mtihani kwa kupata first class. Alibahatika kwenda ng'ambo kuendeleza masomo yake (uk. 28).

Mwenye **hekima**. Mazungunzo ya Sara katika tamthilia hii yanaonekana kuwa yenye wingi wa hekima na busara. Anatoa ushauri katika masuala mbalimbali kama vile: masuala ya ndoa, maisha, heshima na mengineyo.

Mwanamke anaonekana kama **mzazi** anayestahili kujifungua **watoto wa kike na wa kiume** na hasa watoto wa kiume. Asipopata watoto wa kiume, anasutwa na kukejeliwa. Tunaelezwa kwamba Sara alisutwa na kutukanwa na wanajamii kwa kukosa mtoto wa kiume hata baada ya kujaliwa na mabinti watatu baada ya muda mrefu bila watoto (uk. 6,7).

**Mvumilivu** na anayestahili kuvumilia mateso na bughudha za ndoa. Kwa mfano, Sara anavumilia ndoa yake ambayo ilikuwa na changamoto nyingi. Aidha anavumilia mumewe Yona baada ya kumtesa na kumchapa kichapo cha mbwa. Neema anapewa mawaidha na mama yake kuhusu kuzidi kuvumilia ndoa yake. Kudhihirisha suala hili la uvumilivu wa ndoa tunamwona Neema akimweleza mumewe kwamba anakubaliana na wazo kuwa hawaishi katika ndoa ya raha mustarehe mia fil mia (uk. 48). Wazo hili linaonyesha kuwa Neema pia anavumilia ndoa yake na Bunju.

Mtu anayestahili kujukumika katika **majukumu ya nyumbani**. Anasawiriwa kama mtu mwenye majukumu ya shambani, jikoni na nyumbani kwa jumla. Yona anapomkuta Sara ameketi, analalamika kuwa hajaandaliwa chochote. Inambidi Sara amtumie salamu Dina ili aje amsaidie kupika. Hali hii inaonyesha kuwa ni jukumu la mwanamke kupika na kuandaa chakula kwa mumewe.

**Asiyestahili kupata elimu.** Sara anasema kuwa siku zao elimu ya wasichana ilifanywa bezo. Yeye aliachia darasa la saba (uk. 33).

**Kiumbe dhaifu**. Kiumbe ambacho hakifai kushindana na mwanamume. Sara anamwambia bintiye Neema kuwa utamaduni ungali una nguvu na hawezi kushindana na mwanamume (uk. 66).

**Mwenye msimamo dhabiti**. Sara na binti zake wamesawiriwa kama wenye msimamo imara. Kwa mfano, Sara anasimama na familia yake hata baada ya kutukanwa na kukejeliwa na wanajamii. Hakuwacha familia yake, alisimama nayo hadi wakati wa mwisho. Asna pia ana msimamo wake kuhusu ndoa (uk. 53). Anashikilia msimamo kuwa ndoa ni taasisi inayomkandamiza mwanamke na kuwa haifai.

**Karimu**. Dina anaenda kumsaidia Sara kupika kwani yeye ni mgonjwa.

**Msaidizi**. Sara alisaidia Yona kulea na kusomesha watoto alipofutwa kazi.

**Mvivu**. Asna alisema hapendi

**Mlezi**. Sara anawaleo binti zake na Neema pia anatarajiwa kusaidia Lemi homework.

**Msamehevu**. Neema anamsamehe Yona kwa ukatili aliowafanyia

**Mcha Mungu** . Neema anaambia Sara na Asna wakiwa hospitalini kuwa Mungu ndiye huponya. 42

**Mwenye shukran.** Sara anashukuru Mungu kwa watoto aliojaliwa. Neema anashukuru Bunju

**Mwenye utu**. Dina kusaidia Sara

Anakejeliwa. Asna kumwambia Sara kuwa hajui maana ya tomboy kwani hajasoma

**Mtumwa**. Sara anamwambia Dina kuwa kazi zote za nyumbani ni zake.

**Msomi**. Salome anapata first class. Neema ana digrii. Asna amesoma

**Mbishi**. Neema, Asna

**Mwenye upendo**. Sara alivumilia mateso ya Yona kwa upendo wa wanawe ili wapate maisha bora baadaye.

**Amekengeuka**. Asna kuwa tomboy na hataki kuolewa

**Kielelezo cha bidii**. Neema anafanya kazi ya kompyuta, analea Lemi, anashughulikia ugonjwa wa Sara, ni mke nk uk18 Sara anasema mwanamke ana mengi ya kushika na yote yanamtaka ayashike sawasawa.

**Chombo cha maendeleo.** Neema ana gari na shahada mbili

**Mbegu ya mageuzi**. Asna na Neema wanapinga mila hasi zinazozuia mama mkwe kulala kwa mkazamwana

**Mwajiri**. Neema kuajiri Bela. Zozote 20

**Au**

3. ''Nimevaa vizuri na kuivisha tabasamu ila ndani viraka na huzuni tele''

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

Ni maneno ya Bunju

Anamwambia Neema.

Wapo nyumbani mwao- Bunju na Neema

Ni baada ya Neema kumwomba Bunju pesa ili amtibu mamake Sara ndipo Bunju anamjibu.

ii. Tambua mbinu moja ya kimtindo iliyotumika katika dondoo hili. (alama 1)

Jazanda- ndani ni viraka- viraka ni jazanda ya vikwazo anavyo maishani.

Kinaya- kuvaa vizuri lakini ndani ni viraka

iii. Fafanua sifa zozote tano za msemaji wa dondoo hili. (alama 5)

**Bunju**

- Mpenda haki- anamruhusu mkewe kutumia pesa na familia yake
- Mwenye mapenzi- anapenda familia yake na anawakimu.

- Mwenye bidii- kazini - hana muda wa starehe
- Mtamaduni- anashikilia mila km mama mkwe asilale kwao.
- Msiri- mkopo
- Karimu- kulipia Neema bili hata bila kumjua.
- Mwenye mtazamo finyu kuhusu elimu- nambari ni muhimu kuliko alama.
- Mwenye utu- alisaidia Neema alipopata ajali na kumlipia

iv. Kwa hoja zozote kumi, eleza mambo yanayomjaza msemaji viraka. (alama 10)

- Gharama ya kodi kuwa juu
- Ana mkopo wa benki.
- Kulipa karo- ~~Mina~~ anasomea boarding
- Kugharamia chakula
- Kugharamia mavazi
- Kugharamia matibabu ya familia.
- Ametumia pesa kumnunulia Neema gari
- Amelipa karo ya Salome.
- Kuwajengea wazazi wa Neema nyumba.
- Anahisi anakosewa heshima na Neema.
- Kazi nyingi

## SEHEMU C: RIWAYA: Nguu za Jadi: Clara Momanyi

**Jibu swali la 4 au 5**

**4.** a. 'Mimi ni mwanamume. Ninaweza kuoa wakati wowote na idadi yoyote ya wanawake. Shida iko wapi? Mwanamke akishaolewa, basi. Yake yamekwisha hapo. Azae na kuitumikia jamaa yake bila kuulizauliza maswali.'

**i.** Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

Ni maneno ya Mrima.

Anamjibu Mangwasha mkewe.

Wako nyumbani kwao.

Mangwasha alimuuliza ikiwa Sagilu anamtafutia mke mwingine kisiri.

**ii.** Fafanua sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)

**Mrima**

- Mtamaduni- anasema mila hairuhusu yeye akatunzwe na mke kama mgonjwa.
- Mbadhirifu- anafuja pesa na mwanamke nje ya ndoa.
- Mzinzi- ana mwanamke nje ya ndoa- kutoka kwa barua.
- Hajawajibika- anatoweka nyumbani na kumwachia Mangwasha majukumu ya nyumbani.
- Nadhifu- alivaa na kubadilisha suti kila uchao.
- Mcheshi- akikosekana kazini watu waliteta.
- Karimu- alihudumia watu bila uchoyo.
- Mwenye bidii- biashara ya uchuuzi na duka
- Mbaraza- mtu wa watu
- Mlevi- anakesha vilabuni vya pombe.

(b). Maudhui ya usaliti yamejadiliwa kwa kina. Thibitisha. (alama 10)

- Mtemi Lesulia amesaliti mchi kwa kuzorotesha uchumi kupitia ufisadi na sera mbovu
- Mtemi Lesulia amesaliti jamii ya Waketwa kwa kuibagua katika ajira inayowaendea Wakule pekee.
- Mtemi Lesulia amesaliti uaminifu wa Ngoswe kwa kuwaambia vijana wenzake wavuruge amani wakati wa uchaguzi ili ushindi umwendee Sagilu bila kujali usalama.
- Mtemi Lesulia amesaliti hakimu kwa kumnyang'anya cheti na kumfuta kazi licha ya kufanya kazi kulingana na sheria.
- Mtemi Lesulia amesaliti imani ya marafiki zake kwa kuwafukuza walipofika kwake kumpa pole kwa kushindwa kwenye uchaguzi.
- Sagilu amesaliti jamii ya Waketwa walioishi Matango kwa kushiriki kuchoma makazi yao licha ya kuwa alitaka achaguliwe kama mbunge.
- Sagilu amesaliti Mrima kwa kumhonga pesa ili ashiriki ulevi akijua kuwa alimtaka mkewe Mrima mapenzi.

- Sagilu amesaliti Mangwasha kwa kumtembelea akijifanya anajali lakini ndiye alifadhili mumewe Mrima ashiriki ulevi hadi akafutwa kazi.
- Sagilu amesaliti anamsaliti mwanaye Mashauri kwa kumnyang'anya mchumba Cheiya.
- Sagilu amesaliti Mtemi Lesulia kwa kumhakikishai kuwa kila kitu kiko shwari katika uchaguzi huku akijua kuwa hangeshinda.
- Sagilu amesaliti Mtemi Lesulia kwa kuzaa na mkewe Nanzia huku akijifanya rafiki yake
- Sagilu amesaliti jamii ya Matuo kwa kuwauzia watoto maziwa yenye sumu bila kujali ingewadhuru vipi.
- Cheiya anamsaliti mchuimba wake Mashauri kwa kujihusisha kimapenzi na Sagilu babaye Mashauri.
- Nanzia anasaliti jamii ya Matuo kwa kuhodhi mali ya umma kwa manufaa yake binafsi./ kuchoma makazi yao ili afaidi ardhi.
- Nanzia anasaliti mumewe Mtemi Lesulia kwa kufanya mapenzi na Mhindi na Sagilu
- Mbwashu anasaliti Mtemi Lesulia kwa kumtororka na kwenda Ulaya anaposhindwa na walifanya maovu mengi pamoja.
- Chifu Mshabaha anasaliti Waketwa kwa kushiriki njama ya kuwaondoa makao yao.
- Chifu Mshabaha anamsaliti Manwasha kwa kuleta msichana mwingine kazini ili kumfuta yeye kazi.
- Mrima anasaliti mkewe Mangwasha kwa kushiriki mapenzi nje ya ndoa./ anashirikiana na Sagilu huku mkewe akiteseka.
- Mrima anasaliti Mangwasha na akina Lonare anapochukua hongo ili amfanyie Mtemi Lesulia kampeni ilhali anajua huyu ni adui ya Waketwa. **Nk nk zozote 10**

**Au**

5. Matatizo ya Afrika ni tokeo la uongozi mbaya. Thibitisha kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 20)

- Uhaba wa ajira- vijana waliokamilisha masomo wanakosa ajira na wengine wanaonekana na Mangwasha wakiwa katika maeneo ya maduka wakipitisha wakati.
- Kufutwa kazi kiholela- Mangwasha anafutwa kazi bure katika ofisi ya chifu Mshabaha kwa kuunga mkono Lonare.
- Ukiritimba wa kiuchumi- wenye ushawishi kama aikan Sagilu wanamiliki nyenzo zote muhimu za kiuchumi k mashamba, vituo vya petrol na msururu wa maduka ya jumla.

- Unyakuzi wa ardhi- Sagilu na Lesulia wanapanga njama ya kunyakua ardhi ya Wanamatongo badala ya kuwatetea.
- Unyakuzi wa mali ya umma- Nanzia mkewe Mtemi Lesulia ananyakua jingo moja refu katikati yam ji na kubadilisha jina kuwa Skyline Mall.
- Ubaguzi- utawala wa Lesulia kuajiri tu Wakule hata wale hawajahitimu vilivyo na kubagua Waketwa.
- Ukabila- Mshabaha kuajiri watu wengi wa kabila lake
- Kunyanyasa wapinzani- magari ya Lonare yanashikwa bila hatia ila ni kwa sababu anampinga Mtemi Lesulia.
- Uharibifu wa mazingira- matajiri wanachimba mawe na wengine kumiliki karakana za machimbo yam awe.
- Ufisadi/ hongo- chifu Mshabaha anapokea hongo ili aridhiane na serikali ya Mtemi Lesulia kuinyakua ardhi ya Matango kufuatia misingi ya kisiasa.
- Kuchoma nyumba- nyumba za Waketwa kama vile Mangwasha zinachomwa kwa misingi ya kikabila na kisiasa.
- Mishahara duni- Mangwasha anapata mshahara usiokimu familia yake.
- Bidhaa ghushi- Sagilu anaagiza maziwa yaliyotiwa sum una kuhatarisha maisha ya watoto wengi.
- Biashara haramu- madanguro
- Ukosefu wa haki kuamua kesi- Mafamba ni wakili laghai wa serikali- inashinda kesi mbalimbali
- Utekaji nyara- utawala wa Lesulia unamteka nyara Lonare ili asishindane naye katika uchaguzi.
- Kutumia vijana kuzua vita- Lesulia kuwapa vijana fedha ili wahonge watu siku ya uchaguzi na kuzua fujo katika vituo vya Majengo na Matango ambavyo vilikuwa na ufuasi mkubwa wa Lonare.
- Siasa za chuki- Lesulia hakutaka upinzani ndio maana ana chuku kwa Lonare mpinzani wake.
- Mfumuko wa bei- bei ya bidhaa muhimu imepanda katika nchi ya Matuo na kuwafanya watu wa tabaka la chini kama Mangwasha kushindwa kuzimudu.
- Ulanguzi wa mihadarati- Ngoswe, mwanawe Mtemi na watu wengine wenye ushawishi wanamiliki mtandao mkubwa wa ulanguzi wa dawa za kulevya na kudhuru afya za wananchi.

- Mauaji ya kisiasa- Cheiya anatumwa na Mtemi Lesulia kumuua Lonare kwa kumtilia sumu katika kinywaji lakini hakufaulu kwani Lonare hatumiikinywaji hicho.
- Viongozi kutolipa ushuru- Sagilu halipi ushuru na hivyo kuhujumu kipato cha nchi.
- Kuajiri watu wasiohitimu- wasihitimu wanatoa huduma duni kwa wananchi

zozote 20x1

**SEHEMU D: HADITHI FUPI: Mapambazuko ya Machweo na hadithi nyingine.**

**Jibu swali la 6 au 7**

**NIPE NAFASI**

**6. i.** Jadili ufaafu wa anwani ya hadithi hii. (al 10)

- Mama Kazili kuomba nafasi ya kazi ya ajira ili awakimu watoto wake.
- Mama Kazili kuomba nafasi ya kusomesha katika shule ya msingi.
- Mama Kazili kuomba nafasi ili uraia wake wa Lesotho uzidi kutambulika.
- Mama Kazili kuomba nafasi ya kusaidiwa kiuchumi na Moshe.
- Mama Kazili kuomba nafasi ya kukaa na watoto kwa jamaa ya mumewe kwa miezi miwili
- Matweba na wanaume wenzake wanaomba nafasi ya kuzilinda tamaduni na desturi na kusimamisha familia ya Belo
- Moshe anaomba nafasi ya kufanya kazi katika migodi ya Afrika Kusini.
- Mwanaume anuiaye kumuua mkewe aliyemuita mzembe aomba nafasi ya kumuadhibu.
- Wanawake wazee wanaomba nafasi ya kutetea msimamo wa wazee kuhusu utamaduni.
- Wanaume - kutoa maamuzi katika jamii bila kuingiliwa na wanawake. Kazili asieleze namna mwanamke anavyofaa kupigania haki zake.
- Wanawake wa makamo wanaomba nafasi ya kumuunga mkono Kazili kuhusu msimamo wake kwa utamaduni.
- Watoto wa Kazili walipata nafasi ya kusajiliwa shuleni.
- Mama aliyeita mumewe mzembe anaomba nafasi ya kumkosoa mumewe

- Kazili na wanawe wanaomba nafasi ya kupata chakula kwa familia ya Belo.
- Mkhathini anaomba nafasi ya kuishi lakini anaikosa
- Wafugaji farasi wanapata nafasi ya kuokoa maisha ya Kazili na mwanawe
- Wanawake - kufanya mambo bila idhini ya waume zao.
- Wazazi wa Moshe- wachukue pesa anazotuma wala si mkewe. Hata hivyo hawampatii
  - Zozote 10

ii. Fafanua hatua ambazo wanawake wanafaa kuchukua ili kukabiliana na changamoto zinazowakumba. (alama 10)

- Kujibidiisha- mama Kazili anapanda mlima Maloti akiwa amebebba kitoto katika theluji kali.
- Kuwa makini -mama Kazili kupanda milima ya theluji bila kuanguka ovyo.
- Kuripoti- kuripoti Moshe kwa wazazi kuwa ana mke mwingine.
- Kufanya kazi- Mama Kazili ni mwalimu wa shule ya msingi ambako anajipatia mshahara wa kuendeleza familia yake.
- Kutumia busara- mama Kazili kutoa kaulli zilizowafanya wanaume kubaki vinywa wazi na kurejea kwenye Kraal kutoa uamuzi.
- Kutafuta ajira- mama Kazili kutafuta ajira alipopeleka watoto kwa jamaa yake.
- Kuvunja sheria kandamizi- kuondoka bila ruhusa ili kutafuta chakula
- Kuwa jasiri – kubeba maiti kwa kilomita kadhaa
- Kulia- Mkhathini anapofariki ili kutakasa hisia zake
- Kukopa pesa- Mama Kazili alikopa ili kusafiri huko milimani
- Kutafuta msaada- wa chakula kutoka kwa jamaa za mumewe.
- Kuzindua wake wengine-wasikae tu bila kuchukua hatua
- Kuwa na msimamo dhabiti

- Kufahamu haki zao- kuwa raia halali wa Lesotho kupitia ndoa- anapoamuriwa arudi kwao.

- Kuwa wakakamavu

zozote 10

AU

**MSIBA WA KUJITAKIA**

7. i. Matatizo yanayowakumba wahusika katika hadithi ya Msiba wa Kujitakia ni ya kujitakia. Thibitisha. (alama 10)

- Kukosa kibarua- Machoka anapitia magumu kwa kukosa kibarua ilia pate kitu cha kutia mdomoni kwani walichagua viongozi bila kuzingatia vigezo vifaavyo.
- Kusahauliwa na kukumbwa na dhiki- akina Zuhura walichagua kiongozi wa ukoo wao hata kama hafai.
- Kutengwa na viongozi- wakazi wa Matopeni wanaruhusu jimbo lapo kugeuzwa ngome ya watu fulani wanaowania uongozi.
- Wanamatopeni wanampuuza Fumo Matata anapowakumbusha kuwa si busara kuwachagua viongozi kwa kuzingatia koo na sasa wanataabika.
- Kusalia kuwa mpinzani- Zuzu Matata anakataa kuchukua hatamu za uongozi na kumruhusu mzee Sugu Senior kuingoza Matopeni na nafasi yake ya kuongoza ikawa ndoto tu.
- Wananchi kukubali kukandamizwa na kutengwa- uwanjani wakimsubiri kiongozi wanaumizwa na jua huku viongozi wakitengewa nafasi kwenye hema.
- Kutozwa ushuru wa juu- Wanamatopeni wnalalamika kutozwa ushuru na serikali na wao waliichagua.
- Kupanda kwa gharama ya maisha- raia wanalalamika kuhusu mfumuko wa bei ila wao ndio waliwachagua viongozi wasiowajibika.
- Serikali inaaibika kwani viongozi wan chi zingine walioalikwa hawakuhudhuria kwani uchaguzi ulukuwa wa wizi.

- Aibu kwa Sugu Junior kwani viti vilibaki wazi siku ya kuapishwa na sababu ni kuwa ulikuwa ushindi wa bandia wa wizi wa kura. 10x1

ii. 'Akilini mwake anakumbuka shairi alilowahi kulisoma ingawa hakumbuki wapi.'

a. Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

Haya ni maneno ya mwandishi.

Anamrejelea Machoka.

Machoka yu nyumbani kwake ameketi kochini.

Alikuwa amechoka baada ya kutafuta kazi mchana wote bila mafanikio na sasa anawaza kuhusu maisha yake yenye ufukara. 4x1

b. fafanua ujumbe unaojitokeza katika shairi ambalo mrejelewa analikumbuka akilini. (ala 6)

- Kuwazindua wananchi wafungue macho- wane shida wanazopitia.
- Dini- anaomba siku moja Rabana awakarimie.
- Utabaka- wanazidi kufilisika huku viongozi wakitajirika.
- Utamaushi- amechoka kwa sababu ya visanga.
- Majuto- wanajua walijitakia msiba kwani hauna kilio.
- Umaskini- maskini wanataka kugutuka na waone kwani macho yao yatakuwa yamefunguka
- Tumaini - macho yao yatakuwa yamefunguka 6x1

## SEHEMU E: USHAIRI

### 8. SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI

1. Tunda la elimu zote, wanasema wanazuoni

   Ni kwamba mtu apate, kumtambua manani

   Ndipo hadhi apate, akumbukwe duniani.

2. Elimu bila ukweli, haizidi asilani
   Giza na nuru muhali, katu havitangamani
   Uwongo ufe kweli, itue nuru moyoni

3. Elimu ni kama mali, haichoshi kutamani
   Ni bora yashinda mali, taji la wanazuoni
   Elimu njoma miali, langazayo gizani.

4. Mtu hachomwi na mwiba, na viatu miguuni
   Ulimwengu una miiba, tele tele majiani
   Elimu ukiishiba, u salama duniani.

5. Wafu ni wasiosoma, watazikwa ardhini
   Hai ndio maulana, wapaao maangani
   Elimu jambo adhima, aso nayo maskini.

6. Toa wakfu ujana, elimu ukitamani
   Na uwe mzee sana, kujua usijihini
   Elimu ni jambo adhima, aso nayo maskini

7. Elimu ina malipo, utoyalipwa mwishoni
   Pale uitafutapo, ujira usitamani
   Mwanachuoni afapo, mbingu huwa na huzuni.

8. Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachuoni
Wao wameongolewa, na ni taa duniani
Kweli wanapoijua, watoe bila kuhuni.

9. Elimu bila amali, mti usio majani
Haumtii kivuli, aukaliaye chini
Inakuwa mashkeli, wa kughuri insane.

**majibu**

a) Fafanua ujumbe mkuu/ dhamira katika shairi hili. (alama 2)

Ni kuonyesha umuhimu na manufaa ya kupata elimu kama vile kumfanya mtu awe wa kutegemewa, adabu na aliyewajibika.

b) Taja aina na bahari ya shairi hili kutegemea; (alama 3)

idadi ya mishororo katika kila ubeti – tathlitha kwani kila ubeti una mishororo mitatu

idadi ya vipande katika kila mshororo- mathinawi kwani lina vipande viwili kila mshororo

mpangilio wa vina – ukara- vina vya mwisho na sawa na vya kati vinabadilika kiubeti

c) Jadili jinsi mshairi ametumia idhini yake. (alama 3)

Inkisari ½ aso badala ya asiye 1

Kufinyanga sarufi ½ Elimu ukiishiba badala ya ukiishiba elimu 1

d) Fafanua maudhui katika ubeti wa tatu na wa saba. (alama 4)

**Ubeti wa tatu**

Elimu ni kitu cha umuhimu sawa na mali ambayo mtu anatamani.

Elimu inashinda mali na hata ni bora kushinda shahada ya chuoni

Elimu hutoa mwangaza katika giza.

**Ubeti wa 7**

Elimu inakulipa baada ya kuipata

Wakati unasoma/ unatafuta elimu usitarajie mambo yawe mepesi. Mwanafunzi akifa, watu wote huhuzunika

e) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya tutumbi/ nathari. (alama 3)

Mwandishi anasema elimu ambayo haina matokeo/faida ni sawa na mti ambao hauna matawi. Itakuwa haimstiri mtu aliyeketi chini kutokana na jua yaani hapati kivuli. Elimu isiyosaidia/bila faida inakuwa na kasoro kwa kumwendeleza binadamu

f) Eleza toni, nafsi- neni na nafsi nenewa katika shairi hili. (alama 3)

Toni- kushauri, kusihi na kuadilisha

nafsi- neni – msomi, mshauri au anayeelewa umuhimu wa elimu

nafsi nenewa- watu wote/ wanafunzi

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 2)

i. Adhima- heshima

ii. Wameongolewa- wana tabia nzuri